# MUISLAM MDOGO

Kitabu ndogo ambayo imekusanya misingi ya dini ya uislam akhlaaq za mtoto wa kiislam

alsarhaan.com

mahadsunnah.com

بسم الله الرحمن الرحيم

# 1

## KIFUNGU CHA KWANZA

# IMAANI YANGU

### Mimi ni muislam

ALLAAH NI MOLA WANGU.

NA MUHAMMAD SWALLA ALLAAHU ALEYHI WA SALLAM MTUME WANGU.

NA UISLAM DINI YANGU.

### Mimi nampenda Allah aliyetukuka.

KWA SABABU YEYE NI MOLA MLEZI, MWINGI WA REHMA MWENYE KUREHEMU MFALME WA SIKU WA MALIPO.

NA KWA SABABU YEYE AMENIUMBA NA AKANIRUZUKU NA AKANIJAALIA KUWA MUISLAM.

### Allah Amesema:

*KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU* **1** *SIFA NJEMA ZOTE NI ZA MWENYEZI MUNGU, MOLA MLEZI WA VIUMBE VYOTE* **2** *MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU* **3** *MWENYE KUMILIKI SIKU YA MALIPO* **4** *WEWE TU TUNAKUABUDU, NA WEWE TU TUNAKUOMBA MSAADA* **5** *TUONGOE NJIA ILIYO NYOOKA* **6** *NJIA YA ULIO WANEEMESHA, SIYO YA WALIO KASIRIKIWA, WALA WALIO POTEA* **7**

*SURAH AL-FATIHA*

Na ninampenda Mtume ﷺ

Kwa sababu Allah alimtuma kwetu akatutambulisha kwa Allaah na akatufundisha Qur-aan.

Na kwa sababu yeye Mtume swalla Allaah aleyhi wa salaam mpole mwenye huruma , tabia zake tukufu, na sifa zake nzuri.

Allah Amesema:

**Na hakika wewe una tabia tukufu.**

Surah Al-Qalam 68:4

**Allah Amesema:**

**Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.**

**Surah At-taubah 9:128**

## Allah Amesema:

Hakika tumekupa kheri nyingi 1 Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi 2 Hakika anaye kuchukia ndiye aliye mpungufu 3

## Surah Al-kauthar

**Na naipenda dini yangu ya uislam.**

Na kwa sababu ndio dini ya haqq ambayo Allaah ameiridhia kwetu na akaja nayo mtume swalla Allaah aleyh wa sallam.

Na kwa sababu mwenye kushikamana nayo ataingia peponi na mwenye kuiacha ataingia motoni

Allah Amesema:

Naapa kwa Zama 1 Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara 2 Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubir 3

Surah Al-qsr

## Na nguzo za uislam ni tano.

1. Shahada ya kwamba hamna mola apasae kuabudiwa kwa haqq isipokuwa Allaah na Muhammad ni mtume wa Allaah.
2. Kusimamisha swala
3. Kutoa zakaa
4. Kufunga mwezi wa ramadhani
5. Kuhiji nyumba ya Allaah tukufu

## Na nguzo za Imani ni sita

1. Kumuamini Allaah
2. Kuamini malaika
3. Kuamini vitabu
4. Kuamini mitume
5. Kuamini siku ya mwisho.
6. Kuamini qadar kheri yake na shari yake.

**Na napenda yote anayoyapenda Allaah na mtume wake.**

**Na nachukia yote anayoyachukia Alllah na mtume wake.**

# 2

## Kifungu cha pili
## Swala yangu

Allaah ametuumba kwa ajili ya kumuabudu peke yake pasi na kumshirikisha, basi hatumuabudu asiyekuwa yeye wala hatumuombi asiyekuwa yeye.

**Na ibada kubwa ni**
# Swala.

# Na swala ni tano

| | | |
|---|---|---|
| Swala ya asubuhi | 2 | Naswali rakaa mbili |
| Swala ya asubuhi | 4 | Naswali rakaa nne |
| Swala ya alasiri | 4 | Naswali rakaa nne |
| Swala ya magharibi | 3 | Naswali rakaa tatu |
| Swala ya ishaa | 4 | Naswali rakaa nne |

Na nazihifadhi swala kwa wakati wakati wake na nazitekeleza kwa unyenyekevu

Na natawadha kabla ya kuswali na wala siswali bila ya udhu.

# 3

## KFUNGU CHA TATU
# TABIA ZANGU



NA ALLAAH ANAPENDA TABIA NZURI NA ANACHUKIA TABIA MBAYA.
NA MTUME AMEKUJA KUTIMIZA TABIA NZURI.

**BASI JUU YANGU KUJIPAMBA NA TABIA NZURI**

**KAMA UKWELI, UAMINIFU, USHUJAA, UKARIMU, MANENO MAZURI, KUMUHESHIMU MWALIMU, NA KUMUHESHIMU MKUBWA.**

**NA KUJIEPUSHA NA TABIA MBAYA.**

**KAMA UONGO, NA KHIYANA, NA UNYONGE, NA UBAKHILI, NA MANENO MAOVU, NA KUTOHESHIMU.**

**AMESEMA MTUME:**

> HAKIKA YULE AMBAYE YUPO KARIBU NA MIMI KATIKA NAFASI SIKUYA QIYAMA MWENYE TABIA NZURI DUNIANI

# HITIMISHO

- ELIMU NI NURU NA UJINGA NI GIZA.

- BASI NINAJITAHIDI KATIKA KUITAFUTA ELIMU NA NINATOA JUHUDI ZANGU KATIKA KUITAFUTA ILI ANIRIDHIE MOLA WANGU NA ANIINGIZE PEPONI.

- NA ADHKAAR NI KINGA KWA MUISLAM

  BASI NINADUMISHA KULETA ADHKAAR ZA ASUBUHI NA JIONI MIONGON MWAO: KUSOMA AAYATUL KURSIY NA SUURATUL IKHLAASW NA MUAWWIDHATEYN.

- NA DUA NI UFUNGUO WA KUFAULU

  BASI MUOMBE ALLAH SANA KATIKA KILA WAKATI: KATIKA SIJDA NA BAADA YA ADHAN NA USIKU.

## NA MIONGONI MWA DUA

EWE ALLAAH NIONGOZE NA NIJAALIE KUPATIA.

EWE ALLAAH NIZIDISHIE ELIMU

EWE ALLAAH NISAMEHE NA WAZAZI WANGU NA UWAREHEMU.

EWE ALLAAH NIPE DUNIANI MAZURI NA AKHERA MAZURI NA NIKINGE NA ADHABU YA MOTO.

Kitabu ya Muislamu Mdogo, kitabu katika lugha ya kiswahili, kutoka tovuti ya ' nacheza na nasoma' ambaye iko chini ya usimamizi wa Sheikh Heitham Sarhaan, na ni kitabu ndogo inayoongea kuhusu chanzo cha Uislamu na tabia ya mtoto muislamu, imekuja kwa njia ya kupendeza, na inaleta furaha na inavutia kusoma kitabu.